# Jarida la eGA

## Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo la 9 | Julai - Septemba 2024

# MIAKA 10 ya Mfumo wa baruapepe Serikalini (GMS)

Wadau wafurahishwa na Uhakika wa Mawasiliano Salama Serikalini

ega_tanzania    ega online tv

# Yaliyomo

Miaka 10 ya Mfumo wa Baruapepe Serikalini ....................2
Serikali yajipanga kupunguza pengo la kidijiti Nchini....................4
Vodacom Tanzania yatembelea RIDC....................5
Wakuu wa Idara na vitengo vya TEHAMA kushirikiana na Wakaguzi wa Ndani....................6
e-GA yatoa Elimu ya Serikali Mtandao kwa Viziwi....................7
e-GA yaleta mageuzi ya Kidijitali Serikalini....................8
Halmashauri 12 zapatiwa mafunzo ya Mfumo wa e-Board....................9
Zingatieni Sheria ya Serikali Mtandao katika Ukaguzi wa Mifumo : Mwamnyasi....................10
Ushirikiano wa TPA na e-GA wachochea matumizi ya TEHAMA Bandarini....................11
Mazinigira wazeshi yatajwa kuchochea ukuaji wa Serikali Mtandao Nchini....................12
e-GA yapongezwa ujenzi wa Mifumo ya Kielektroniki Serikalini....................13
Wahamasisheni wadau kutumia Mfumo wa e-Mrejesho : e-GA ....................14
Jifunzeni Teknolojia Mpya kwa maslahi ya Taifa : Mhandisi Ndomba....................15
Matukio katika picha ....................16



## Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu

Karibu katika toleo la tisa la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika jarida hili utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za Serikali Mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini, inayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma bora kwa umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utaweza kufahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nichukue fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

Nakutakia usomaji mwema.

Mhandisi Benedict B. Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

# MIAKA 10 YA MATUMIZI YA MFUMO WA BARUAPEPE SERIKALINI (GMS)
# WADAU WAFURAHISHWA NA UHAKIKA WA MAWASILIANO SALAMA SERIKALINI




Lilianza kama wazo, kisha wataalamu wakaketi na kutengeneza mfumo wa Baruapepe Serikalini (Government Mailing System - GMS), ambapo sasa umetimia muongo mmoja wa mafanikio ya matumizi ya mfumo huu.

Kwanini tusijenge mfumo wa baruapepe Serikalini, ili kila mtumishi wa umma aweze kufanya mawasiliano ya kiofisi kupitia mfumo huu? Hili ndilo swali lililoifanya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kusanifu na kujenga mfumo wa GMS mwaka 2014.

Dhamira kubwa ya ujenzi wa mfumo huu ni kurahisisha mawasiliano kati ya taasisi za umma, sambamba na kuimarisha usalama wa taarifa za serikali katika dunia hii ya Sayansi na Teknolojia ambapo, TEHAMA ni nyenzo muhimu na wezeshi katika utendaji kazi wa shughuli mbalimbali za taasisi.

Pamoja na kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA, suala la usalama wa taarifa ni jambo muhimu sana kwakuwa, TEHAMA ikitumika vibaya inaweza kuhatarisha usalama wa taarifa za Serikali.

Itakumbukwa kuwa, kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia mawasiliano mengi ndani ya taasisi za umma yalifanyika kwa njia ya barua, njia hii ya mawasiliano ilichukua muda mrefu na hivyo kupunguza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi, e-GA ilisanifu na kutengeneza mfumo wa Buruapepe Serikalini (GMS) kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya mawasiliano katika taasisi za umma.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba anabainisha kuwa, mfumo wa GMS umetengenezwa ili kurahisisha mawasiliano ndani ya taasisi za umma pamoja na wadau wake, ikiwemo kuwawezesha viongozi na watendaji kufanya maamuzi kwa wakati.

Anafafanua kuwa, kabla ya kuwepo kwa mfumo huu, taasisi za Serikali zilitumia mifumo yake binafsi iliyotengenezwa na wakandarasi au baruapepe za muda mfupi 'disposable email' kama Yahoo na Gmail kubadilishana taarifa na nyaraka mbalimbali za Serikali.

"Mifumo hiyo ya baruapepe ilikabiliwa na changamoto mbalimbali za kiusalama kwani utunzwaji wa taarifa hizo haukuwa wazi kwa Serikali kwakuwa hakukuwa na makubaliano yoyote juu ya utunzaji wa taarifa kati ya Serikali na Wakandarasi waliotengeneza mifumo hiyo", anafafanua Ndomba.

Sambamba na hilo, Ndomba anabainisha kuwa, gharama za ununuzi na uendeshaji wa mifumo hiyo ya baruapepe zilikuwa kubwa na ufanisi wake ulikuwa mdogo, changamoto ambazo zimetatuliwa kupitia mfumo wa GMS ambao umeimarisha usalama wa taarifa za Serikali na uhakika wa upatikanaji wa huduma ya baruapepe kwa taasisi zote za umma.

Ndomba ametaja lengo kuu la kutengeneza mfumo wa GMS ni kurahisisha mawasiliano kwa njia ya baruapepe katika taasisi zote za Serikali na wadau wake, pia kuhakikisha usalama wa taarifa na nyaraka zote zinazosafirishwa kupitia mfumo huu.

Katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanza kutumika kwake, mfumo wa GMS umesaidia kuimarisha mawasiliano ya uhakika na salama kwa njia ya baruapepe ndani ya taasisi za umma, na kuziwezesha taasisi kutumia kikoa cha ofisi husika .

Hadi sasa jumla ya taasisi na vituo vya kutolea huduma zaidi ya 700 zinatumia mfumo wa GMS ,zikiwemo Wizara na Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Taasisi za Umma, Mamlaka na Wakala za Serikali pamoja na Halmashauri.

Katika kuhakikisha usalama wa mfumo wa GMS, Ndomba anabainisha kuwa, mfumo huu umehifadhiwa nchini Tanzania katika mazingira salama, vilevile e-GA imeunda timu maalum inayofanya kazi saa 24 kwa siku ili kudhibiti matukio hatarishi ya usalama wa mfumo huu pamoja na mifumo mingine ya Serikali.

Anabainisha kuwa, mfumo wa GMS umetengenezwa na vijana wa Kitanzania waliojengewa uwezo na Serikali kwa kuzingatia teknolojia ya kisasa kabisa, na umeisaidia Serikali kuokoa takribani asilimia 85 ya gharama za uendeshaji ukilinganisha na bei ya soko ya wakandarasi wengine wa nje.

"Mfumo wa GMS hufanyiwa maboresho mara kwa mara kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza, ili kudhibiti usalama wa mfumo pamoja na kukidhi mahitaji ya watumiaji kwakuwa, kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza pia mahitaji ya watumiaji katika mfumo huongezeka na wakati mwingine inatupasa kuongeza features mpya ili kukidhi mahitaji hayo", anasisitiza Ndomba.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA) CPA. Pius Maneno anasema kuwa, mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa barua ndani ya taasisi za umma kwani, awali utumaji wa barua ulikuwa unatumia muda mrefu hadi kufika ofisi iliyokusudiwa na muda mwingine barua hiyo hufika kwa kuchelewa na kuathiri utekelezaji wake.

"Sasahivi kupitia GMS kila taasisi imetengenezewa akaunti maalumu kwa ajili ya kutuma barua, hapa NBAA tunatumia barua@nbaa.go.tz na baada tu ya kubonyeza kitufe cha kutuma, barua hiyo inakuwa imefika sehemu husika bila kuchelewa", anasema CPA. Maneno.

Naye Bw. Salumu Ally Kulindwa, Afisa TEHAMA mwandamizi kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), ameipongeza e-GA kwa kutimiza miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS), na kuishauri e-GA kuimarisha ushirikiano zaidi



kati yake na taasisi nyingine za umma ikiwemo COSTECH.

"Katika miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa GMS, sisi COSTECH tunajivunia sana mfumo huu kwani e-GA imekuwa ikitoa ushirikiano wa haraka pale tunapopata changamoto yoyote katika matumizi ya mfumo huu au hata mfumo mwingine, e-GA hutatua changamoto hizo na kutoa mrejesho kwa wakati", anasema Bw. Salum.

Ameongeza kuwa, COSTECH imekuwa ikipata ushauri kutoka e-GA wa masuala mbalimbali ya TEHAMA na hivyo, ushirikiano huo umekuwa chachu katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA na ujenzi wa Serikali Mtandao.

Magreth Kageya ni Afisa Uhusiano na Mawasiliano Mwandamizi wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA) anasema kuwa, mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa taarifa za Serikali kwa taasisi za Umma, kwakuwa taarifa hizo zinapita mahali salama na pia hata mpokeaji wa taarifa anakuwa na uhakika anapokea taarifa kutoka sehemu husika kwa kuwa, baruapepe zote zinakuja na jina la mtumaji, taasisi pamoja na kikoa cha go.tz.

"Kwasasa usiri na usalama wa taarifa za Serikali umeongezeka, mtumishi anapotuma taarifa mbalimbali zinazohusu Serikali anapata uhakika kuwa taarifa au nyaraka zinapotumwa zinakuwa ni salama na hazitoki nje ya Tanzania na hivyo kudumisha usiri wa taarifa hizo na kulinda maslahi ya taifa letu" anafafanua Bi. Kageya.

Dkt. Adolar Beatus Duwe, Afisa Utumishi Mkuu kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Bohari ya Dawa (MSD) anasema, awali gharama za uendeshaji wa mfumo wa baruapepe katika taasisi za umma zilikuwa kubwa na ikitokea changamoto yoyote ya mfumo ilibidi kumlipa mkandarasi wa nje aliyejenga mfumo huo ili aweze kutatua changamoto husika.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba.

**"Miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ni kutengeneza miundombinu na mifumo shirikishi katika taasisi za umma ili kupunguza urudufu wa mifumo, na sisi tumefanikiwa kwa kutengeneza mfumo huu wa GMS ambao unatumiwa na taasisi zote za Serikali, hivyo kupunguza gharama za uendeshaji kwa Serikali kwa kila taasisi kununua na kuendesha mfumo wake wa baruapepe"**

Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

"Uwepo wa mfumo wa GMS umezisaidia taasisi zote zinatumia mfumo huu shirikishi pindi inapotokea changamoto, e-GA huwa inatoa taarifa kwa taasisi zote za umma na changamoto hizo zinatatuliwa bila gharama yoyote na kwa wakati tofauti na awali tulipokuwa tukitumia baruapepe zilizotengenezwa na wakandarasi", anasema Duwe.

Naye Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA wa e-GA Bw. Ricco Boma anasema kuwa, mfumo wa GMS umehuishwa kutoka GMS 1.0.0 hadi GMS 4.0.0, ili kuuongezea usalama na ufanisi zaidi na umeunganishwa na mifumo mingine ya TEHAMA ukiwemo mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Uendeshaji wa Shughuli za Taasisi (ERMS) na Mfumo wa Ununuzi (NeST).

Aidha, kwaupande wa kuwajengea uwezo maafisa wanaotumia mfumo wa GMS, Mkurugenzi huyo amesema kuwa Mamlaka inatoa mafunzo mbalimbali ya usimamizi wa mfumo huo ikiwa ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo maafisa wa vitengo vya TEHAMA Serikalini, ili waweze kuumudu na kuuendesha mfumo huo kwa ufanisi na ufasaha zaidi.

Meneja wa Huduma za Sheria wa e-GA Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutahiwa, ametoa rai kwa watumishi wote wa taasisi za umma, kutumia mfumo wa GMS, kila wanapofanya mawasiliano ya Serikali kwani kwa kutokufanya hivyo ni uvunjifu wa Sheria ya Serikali Mtandao ya Namba 10 ya Mwaka 2019.

Aidha, Meneja huyo amewataka watumishi wote wanaotumia mfumo wa GMS kuwasilisha changamoto wanazokutana nazo kwa Maafisa **TEHAMA** wa taasisi zao ili ziwasilishwe katika Dawati la Msaada wa kiufundi kupitia mfumo Mfumo wa Huduma kwa Wateja,. ambao unapatikana kupitia https://helpdesk.ega.go.tz saa 24 siku 7 za wiki kwa mwaka (24/7/365) au kwa kupiga simu namba **0764292299 au 0763292299** ambapo watumishi wa dawati hilo watazipokea changamoto hizo na kuzifanyia kazi kisha kutoa mrejesho kwa muhusika.




Meneja Rasilimaliwatu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) Bi. Vumilia Sailen.




Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Xavier Daudi, akizungumza na washiriki wa warsha ya mafunzo ya usimamizi wa huduma za umma na mfumo wa utawala wa data 'Capacity Development and Consultation Workshop on Public Service Management and Data Governance Framework'.

# SERIKALI YAJIPANGA KUPUNGUZA PENGO LA KIDIJITI NCHINI

Serikali imesema kuwa, itaendelea kupunguza pengo la kidijiti lililopo kati ya mijini na vijijini ili kuhakikisha mapinduzi ya kidijitali yanaleta maendeleo chanya na usawa katika maeneo yote sambamba na kuboresha hali ya kiuchumi kwa wananchi.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Xavier Daudi, wakati akifungua warsha ya mafunzo na mashauriano ya siku mbili kuhusu usimamizi wa huduma za umma na mfumo wa utawala wa data 'Capacity Development and Consultation Workshop on Public Service Management and Data Governance Framework' iliyofanyika Agosti 21, jijini Dodoma.

Alisema kuwa, Serikali imeendelea kuwekeza katika teknolojia ikiwemo kuboresha miundombinu ya teknolojia, ujenzi wa mifumo mbalimbali sambamba na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA Serikalini, katika kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia.

"Serikali kupitia e-GA, imeanzisha mifumo inayowezesha wananchi kupata huduma za Serikali kwa urahisi, ikiwa ni pamoja na mfumo unaowezesha wananchi kutuma, kupokea na kushughulikia malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi 'e-Mrejesho', Mfumo wa Malipo Serikalini 'GePG' pamoja na Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi ' MGoV'", alisema Bw. Xavier.

Alifafanua kuwa, katika kupunguza pengo la kidijiti nchini, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma kwa umma, ni moja ya mkakati unaofanywa na Serikali ili kuhakikisha wananchi wote waishio mijini na vijijini, wanapata huduma kwa urahisi na haraka mahali walipo bila ya upendeleo.

Alibainisha kuwa, juhudi hizi zinazofanywa na e-GA zinalenga kuweka mazingira wezeshi ya matumizi ya teknolojia ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali katika maeneo yote pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa watumishi wa umma.

Bw. Xavier alisisitiza kuwa, serikali imedhamiria kuharakisha matumizi ya teknolojia yanazidi kuimarika kwa kuweka mazingira mazuri ya uwezeshaji ya kisera, kisheria pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA katika teknolojia zinazoibukia ili zitumike vizuri na kuleta tija kwa Taifa.

> **"Tunaendelea kuimairisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa TEHAMA kama ambavyo leo tunashuhudia ushirikiano huu kati ya yetu sisi Serikali na Idara ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Kiuchumi na Kijamii (UN DESA), hii inaashiria dhamira tuliyonayo ya kuhakikisha tunafikia malengo ya ujenzi wa Serikali ya kidijiti kwa ushirikiano wa pamoja na taasisi zisizo za kiserikali"**
>
> Bw. Xavier Daudi.
> **Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi. Benedict Ndomba alisema kuwa, e-GA itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kuhakikisha mifumo na miradi ya TEHAMA Serikalini inaleta tija iliyokusudiwa.

Alibainisha kuwa, warsha ya usimamizi wa huduma za umma na mfumo wa utawala wa data 'Capacity Development and Consultation Workshop on Public Service Management and Data Governance Framework' ni muhimu kwa viongozi na Maafisa TEHAMA Serikalini, kwani inawapa elimu juu ya namna ya kusimamia eneo hilo kwa ufanisi zaidi.

Naye Bi. Shabnam Mallick, Mkuu wa Ofisi ya Uratibu wa Makazi Umoja wa Mataifa alisema, matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi Serikalini ni kichocheo kikubwa cha kufikia dhima ya maendeleo endelevu.

Alibainisha kuwa, matumizi ya teknolojia zinazoibukia yatasaidia Serikali kuongeza ufanisi, uwazi na ushirikishwaji katika huduma na hatimaye kuchangia katika maendeleo endelevu ya nchi.

Bi. Mallick amesema, pengo la kidijiti lililopo kati ya mijini na vijijini linazuia uwezo wa kutumia kikamilifu faida zipatikanazo na matumizi ya mifumo ya kidijitali na hata kufikia

" Ili kukabiliana na changamoto hii ya pengo la kidijiti, mbinu za kina zinahitajika ikiwa ni pamoja na uwekezaji wa kimkakati katika taarifa, matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka ikiwemo Akili Mnemba (Artificial Intelligence - AI) na pia Serikali inapaswa kuweka kipaumbele katika ujuzi wa matumizi ya teknolojia" alisema Bi. Mallick.

Warsha ya Usimamizi wa Huduma za Umma na Mfumo wa Utawala wa Data 'Capacity Development and Consultation Workshop on Public Service Management and Data Governance Framework' iliandaliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Idara ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Kiuchumi na Kijamii (UN DESA).



# VODACOM TANZANIA YATEMBELEA KITUO CHA UTAFITI NA UBUNIFU CHA e-GA

Kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya Vodacom Tanzania, imefanya ziara ya kikazi katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), jijini Dodoma na kufanya mazungumzo na e-GA kuhusu namna ya kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili.

Ziara hiyo ya Vodacom ililenga mambo muhimu matatu, ikiwemo kufahamu shughuli na jitihada mbalimbali za e-GA kwenye eneo la utafiti na ubunifu zinazoendelea kituoni hapo, kutoa uzoefu kwenye bidhaa na teknolojia ya Mawasiliano kwa vijana wabunifu waliopo kituoni hapo pamoja watumishi wa e-GA pamoja na kufanya kikao cha kujadiliana kuhusu maeneo mbalimbali ya ushirikiano baina ya Vodacom na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kupitia Kituo cha eGovRIDC.

Aidha, Wawakilishi kutoka Kampuni ya Vodacom walipata fursa ya kutembelea kituo hicho, na kuona tafiti na bunifu zinazofanywa na vijana wenye fani ya TEHAMA, kutoka vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi wanaofanya mafunzo kwa vitendo, mafunzo kazini na wanaojitolea katika kituo hicho.



Watumishi wa kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya vodacom Tanzania, wakiwa katika picha ya pamoja na vijana wanaofanya mafunzo kwa vitendo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika kituo cha Utafiti, Ubunifu na uendelezaji wa Serikali Mtandao jijini Dodoma.

# WAKUU WA IDARA NA VITENGO VYA TEHAMA SERIKALINI WATAKIWA KUWASHIRIKISHA WAKAGUZI WA NDANI KATIKA UJENZI WA MIFUMO YA TEHAMA



Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali Bw. Benjamin Magai, akizungumza wakati wa Mafunzo kwa Wakaguzi wa ndani Mkoani Morogoro.

Wakuu wa Vitengo na Idara za TEHAMA Serikalini, wametakiwa kuwashirikisha Wakaguzi wa Ndani wa taasisi, katika hatua za awali za ujenzi wa mifumo na miradi ya TEHAMA, ili kuhakikisha inazingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Wito huo umetolewa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali Bw. Benjamin Magai, wakati wa kufunga mafunzo maalum kwa Wakaguzi wa Ndani wa taasisi na mashirika ya umma, yaliyofanyika mkoani Morogoro kuanzia Septemba 23 hadi 26 mwaka huu.

**"Kila Mkuu wa Kitengo na Idara ya TEHAMA Serikalini, anapaswa kuhakikisha anawashirikisha Wakaguzi wa Ndani wa taasisi katika hatua zote za ujenzi wa mifumo na miradi ya TEHAMA kuanzia hatua za awali na hata baada ya mifumo hiyo kukamilika ili wakaguzi hao wafanye majaribio kabla ya kuanza kwa matumizi rasmi"**

**Bw. Benjamin Magai**
Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali

Vilevile, Bw. Magai aliwataka Wakaguzi wa Ndani Serikalini kuchukua tahadhari kubwa katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha usalama wa mifumo pamoja na kuzingatia weledi ili kuzuia udukuzi katika mifumo hiyo.

Naye Mwenyekiti wa washiriki katika mafunzo hayo Bw Frank Kindimba ambaye pia ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), ameishukuru Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) pamoja na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yamewajengea uwezo katika usimamizi wa miradi na mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Alibainisha kuwa, mafunzo hayo yamekuwa na tija kubwa kwa washiriki kwani wamepata elimu ya usalama wa mifumo na matumizi sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA.

"Tutakaporejea katika vituo vyetu vya kazi tutazingatia matumizi sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA kwani, katika mafunzo haya hatujasoma Sheria ya Serikali Mtandao pekee bali pia tumejifunza kuhusu usalama na matumizi sahihi ya mifumo", alisema Bw. Frank.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) huendesha mafunzo hayo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali (IAG), ili kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwenye ukaguzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao na kuhakikisha inakuwa na tija kwa Serikali.

**"Kupitia mafunzo haya, washiriki wote tumepata uelewa wa pamoja kuhusu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao na uelewa huu utatusaidia katika kufanya kazi zetu za kikaguzi kwa usahihi zaidi"**

**Bw Frank Kindimba**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani - MUST




Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), akitoa elimu kuhusu Serikali Mtandao kwa viziwi. Kulia ni Mkalimani wa lugha ya alama.

# e-GA YATOA ELIMU YA SERIKALI MTANDAO KWA VIZIWI

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetoa elimu ya matumizi ya Serikali Mtandao kwa viziwi wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Kimataifa ya Viziwi 2024, ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Shinyanga Septemba 23-28 mwaka huu.

Katika kongamano hilo, e-GA ilitoa elimu kuhusu Serikali Mtandao na namna inavyoweza kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kupitia mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa watu wenye mahitaji maalumu wakiwemo Viziwi.

Moja ya mfumo uliowasilishwa ni Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu ya Mkononi (mGov), ambapo mwananchi anaweza kupata huduma mbalimbali za Serikali kupitia simu ya mkononi kwa kupiga namba ya msimbo ***152*00#.**

Akizungumza katika kongamano hilo Afisa TEHAMA kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw.Patrick Mdagano, amebainisha kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao inaendelea kubuni mifumo ambayo itarahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi wa makundi yote katika jamii.

"Kwa kutumia mfumo wa mGov ambao unapatikana hata kwenye simu ya kawaida 'kiswaswadu' kupitia namba ya msimbo *152*00# unaweza kupata huduma za serikali ukiwa mahali popote", alifafanua Bw. Mdagano.

Vilevile, Bw. Mdagano alieleza kuhusu mfumo wa e-Mrejesho unaotumika kama kiungo cha mawasiliano kati ya wananchi na Serikali, na kuwataka Viziwi kutumia mfumo huo kuwasilisha changamoto zinazowakabili katika upatikanaji wa huduma mbalimbali za Serikali, ili ziweze kupatiwa suluhisho kwa haraka katika taasisi husika.

Mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# na kisha kuchagua namba 8 na kisha namba 2, njia zingine ni kupitia simu janja kwa kupakua Aplikesheni (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana kwenye Play Store na Apple Apps Store, na kwa njia ya Tovuti ya emrejesho.gov.go.tz.

Naye Afisa Sheria wa e-GA Bw. Watson Kimbe alisema kuwa, Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, inatambua uwepo wa watu wenye mahitaji maalumu wakiwemo Viziwi katika utoaji wa huduma bora za Serikali Mtandao nchini.

Aliongeza kuwa, kifungu cha 28 (e) cha sheria hiyo kinatoa malekezo kwa taasisi za umma kuweka mazingira rafiki ya utoaji wa huduma za serikali mtandao kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Kwa upande wake Mjumbe wa Bodi ya Utendaji kutoka Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Subira Upurute, ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa jitihada zake za kuyafikia makundi yenye mahitaji maalumu.

"Kwa miaka mingi iliyopita kundi la Viziwi limekuwa ni kundi la mwisho katika kupata taarifa mbalimbali, lakini tunaishukuru e-GA kwa kuwa karibu na kundi hili na kutujengea uelewa kuhusu dhana ya Serikali Mtandao", alisema Bi.Upurute.

Alibainisha kuwa, Serikali Mtandao imewasaidia Viziwi katika upatikanaji wa huduma mbalimbali za serikali ikiwemo ulipaji wa Ankara za umeme na maji kupitia simu ya mkononi.

Aidha,Bi Upurute ameishukuru e-GA kwa kushiriki katika maadhimisho hayo ikiwa ni dhamira ya wazi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, kuunga mkono jitihada za CHAVITA katika kujenga ustawi wa Viziwi katika ulimwengu wa kidijiti.



Baadhi ya washiriki wa kongamano la wiki ya kimataifa ya Viziwi wakifuatilia mada kuhusu Serikali Mtandao wakati wa kongamano hilo.



**Dkt. Said Mohammed** Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania.

# e-GA IMELETA MAGEUZI YA KIDIJITALI SERIKALINI: DKT. SAID MOHAMMED

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) Dkt. Said Mohammed, ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa jitihada inazofanya, katika mageuzi ya kidijitali Serikalini, jambo ambalo limechangia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Dkt. Mohammed amesema hayo hivi karibuni ofisini kwake jijini Dar es Salaam, wakati alipofanya mahojiano maalum na mwandishi wetu kuhusu mchango wa e-GA katika mapinduzi ya kidijitali kwenye taasisi za umma.

Amesema kuwa, NECTA inajivunia sehemu kubwa ya mafanikio ya utoaji wa huduma katika kipindi cha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1973, kutokana na matumizi ya TEHAMA ambayo yamechagizwa na Mamlaka ya Seriikali Mtandao (e-GA).

"Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kumechagiza matumizi ya TEHAMA katika Baraza la Taifa la Mitihani kwenye utoaji wa huduma mbalimbali, kwa watahiniwa ikiwemo hatua za awali za uendeshaji wa mitihani kama vile usajili na utoaji wa vyeti kwa watahiniwa", amefafanua Dkt. Said.

Ameeleza kuwa, NECTA inafaidika na Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) ambao umesaidia katika utendaji wa shughuli mbalimbali za ndani za taasisi kwa kuongeza ufanisi, kwani mzunguko wa majalada hufanyika kwa urahisi na haraka na hivyo kurahisisha utoaji huduma kwa umma.

Ameongeza kuwa, NECTA imekuwa ikitumia Mfumo wa Kujisajili kupitia Mtandao (e-Service), Mfumo wa kuomba cheti mbadala kupitia mtandao na Mfumo wa kundaa matokeo na ripoti ili kusaidia watahaniwa kupata huduma kwa haraka mahali walipo.

Amebainisha kuwa, NECTA hushirikiana na e-GA katika ujezi wa mifumo ya kielektroniki ambayo hutumika katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa ufanisi na wakati .

Ameongeza kuwa, kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, Taasisi za Umma hazina budi kwenda sambamba na mabadiliko hayo kwa kuwekeza zaidi kwenye eneo la TEHAMA na kuimarisha usalama wa nyaraka na taarifa mtandaoni pamoja na mifumo kwa ujumla.

"Ni lazima sisi kama watendaji tuwe tayari kubadilika na kuendana na kasi hiyo kwa kufanya uwekezaji zaidi kwenye TEHAMA na kuangalia usalama wake" Amesema Dkt. Mohammed

Ameongeza kuwa, NECTA imedhamiria kuhakikisha huduma zote zinatolewa kupitia mtandao ikiwemo ufundishaji (e- Teaching na e-Learning) pamoja na utahini kupitia mtandao (e assessment).

"Kutokana na mafanikio tunayoyapata kupitia e-GA, NECTA itandeleza ushirikiano mzuri uliopo ili tuweze kufikia malengo ya taasisi na kurahisisha utoaji wa huduma za umma kwa wepesi na ufanisi zaidi", amesema Dkt. Said.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi, Benedict Ndomba amepongeza jitihada zinazofanywa na NECTA katika matumizi ya TEHAMA kwenye utendaji kazi wake na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Ndomba amesema kuwa, NECTA ni moja kati ya taasisi zilizofanya mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma kidijitali na hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma hizo.

Ndomba ametoa rai kwa Taasisi za Umma kuwekeza katika TEHAMA na kutumia mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma kwa wananchi ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi.

> **"Sisi NECTA tumekuwa tukishirikiana na e-GA katika ujenzi wa mifumo, lakini pia tunashirikiana katika kujengeana uwezo kupitia mafunzo mbalimbali yanayoandaliwa na e-GA yenye lengo la kutusaidia katika usimamizi na usalama wa taarifa (data) kwani, sisi NECTA tumekuwa tukizalisha na kuchakata taarifa nyingi kutokana na Idadi kubwa ya watahaniwa tunaokuwa nao"**
>
> **Dkt. Said Mohammed**
> Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania




Baadhi ya watumishi kutoka Halmashauri mbalimbali wakipata mafunzo kuhusu Mfumo wa e-Board.

# HALMASHAURI 12 ZAPATIWA MAFUNZO YA MFUMO WA e-BOARD

Jumla ya watumishi 49 kutoka halmashauri 12, wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kuratibu Vikao vya Bodi na Menejimenti (e-Board).

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Mamalaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yalifanyika kuanzia Septemba 18 hadi 20 mwaka huu mjini Morogoro, na kuwahusisha Maafisa TEHAMA, Maafisa wanaohusika na kuratibu vikao vya Bodi, Menejimenti na Madiwani, Maafisa kutoka Idara ya Utawala na wajumbe kutoka kwenye Menejimenti.

Akizungumza mara baada ya kuhitimisha mafunzo hayo Afisa TEHAMA kutoka e-GA Bi. Khadija Mzenzi alisema, lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa juu ya matumzi sahihi ya mfumo wa e-Board, ili halmashauri hizo ziweze kuratibu uendeshaji wa vikao vya Bodi, Menejimenti na Madiwani kwa njia ya kidigiti.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo wameipongeza e-GA kwa ujenzi wa mfumo huo ambao unalenga kuongeza ufanisi wa uandaaji na uendeshaji wa vikao sambamba na kupunguza gharama za uendeshaji.

**"Kutokana na mafunzo tuliyopata, Mfumo wa e-Board unadhamiria kutusaidia sisi watendaji kuendesha vikao kwa urahisi zaidi na kutunza kumbukumbu kwa ufasaha"**

**Bw. Yahya Madenge**
**Mkuu wa Idara ya TEHAMA - TEMEKE**

Afisa Tawala Wilaya ya Busega Bw. Meshack John, alisema kuwa, ni vema halmashauri zote zikaanza kutumia mfumo huo ili kurahisisha shughuli za uandaaji na uendeshaji wa vikao ndani ya halmashauri.

Naye Mkuu wa Idara ya TEHAMA Manispaa ya Temeke Bw. Yahya Madenge alisema kuwa, mfumo wa e-Board ni miongoni mwa jitihada znazofanywa na e-GA za kuhakikisha shughuli zote za utendaji kazi ndani ya taasisi za umma zinafanyika kidijiti ikiwemo uendeshaji wa vikao.

Aidha, Afisa ufuatiliaji na tathimini Halmashauri ya Wilaya ya Magu Bi. Christa Manyalla na Katibu wa Mikutano Halmashauri ya Manispaa ya Moshi Gudika kimboka walisema kuwa, mfumo huo wa e-Board utakuwa msaada mkubwa katika kupunguza gharama na kurahisisha uandaaji wa vikao vya Bodi na Menejimenti katika halmshauri hizo.

# ZINGATIENI SHERIA YA SERIKALI MTANDAO MNAPOFANYA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA: MWAMNYASI



Wakaguzi wa ndani katika Taasisi na Mashirika ya Umma wakipata Mafunzo kuhusu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Wakaguzi wa Ndani katika taasisi na mashirika ya umma wametakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ukaguzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA ili kulinda thamani halisi ya fedha za Serikali katika miradi hiyo.

Rai hiyo imetolewa Septemba 23 mwaka huu na Mkurugenzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Msaidizi anayeshughulikia Wizara, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali, kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG) Bw. Paison Mwamnyasi, wakati akifungua mafunzo ya awamu ya saba kuhusu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Wakaguzi wa Ndani wa Serikali yanayofanyika mkoani Morogoro.

Alisema kuwa, lengo la mafuinzo hayo ni kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani katika ukaguzi wa mifumo na miradi mbalimbali ya TEHAMA Serikalini, ili kuhakikisha miradi na mifumo yote ya TEHAMA katika taasisi za umma inazingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kuanzia hatua za awali hadi za mwisho za ujenzi wa miradi hiyo.

> **"Wakaguzi wa Ndani mnapaswa kuhakikisha kuwa taasisi zenu zinazingatia matakwa ya kisheria katika Miradi na Mifumo ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na miradi hiyo kuwasilishwa e-GA ili kupata kibali kabla ya kuanza utekelezaji wake"**
>
> Bw. Paison Mwamnyasi,
> **Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

Alisisitiza kuwa, kaguzi zote za mifumo zinapaswa kufanyika kwa vitendo na sio kwa nadharia na hivyo, ni wajibu wa Maofisa hao kuwa na uelewa kuhusu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili waweze kufanya kaguzi za mifumo ya TEHAMA kwa ufanisi na weledi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Sylvani Shayo, alisema kuwa mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani ili kuongeza ufanisa katika utendaji kazi wao na kushiriki katika ujenzi wa Serikali Mtandao.

"Tunatarajia kuwa, baada ya kupata mafunzo haya, Wakaguzi wote wa Ndani mliopo hapa mtakuwa mabalozi wazuri wa Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao na mtatoa ushauri chanya wenye tija katika taasisi zenu ili kwa pamoja tuweze kuijenga Serikali Mtandao", alisema Bw.Shayo.

Mafunzo hayo ya siku nne yaliratibiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG) yalilenga kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani katika kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha zaidi ambapo jumla ya Wakaguzi wa Ndani 70 kutoka taasisi na mashirika ya umma 49 walipata mafunzo hayo.



Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Sylvan Shayo.



Mkurugenzi wa TEHAMA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Abdulatif Minhajj.

# USHIRIKIANO WA TPA NA e-GA WACHOCHEA MATUMIZI YA TEHAMA BANDARINI

Ushirikiano uliopo kati ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), umechangia kukua kwa matumizi ya Serikali Mtandao katika uendeshaji wa shughuli za bandari na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa TEHAMA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Abdulatif Minhajj, hivi karibuni wakati alipofanya mahojiano maalum na mwandishi wetu kuhusu mchango wa e-GA katika mapinduzi ya kidijitali kwenye Taasisi za Umma ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

Amesema kuwa, e-GA imekuwa ikishirikiana kwa karibu na TPA katika ujenzi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA, ukiwemo Mfumo wa Pamoja wa Kielekroniki wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (Tanzania Electronic Single Window System - TeSWS), ambao huratibu shughuli zote za uondoshaji wa shehena maeneo ya forodha kwa njia ya kidijiti.

“Mamlaka ya Bandari - TPA imeshirikiana na e-GA na wadau wengine katika ujenzi wa mfumo wa TeSWS, mfumo huu umesaidia wateja kuwasilisha taarifa za shehena za mizigo sehemu moja, na taarifa hizi zikafanyiwa kazi kwa haraka zaidi hivyo, kuongeza ufanisi na kupunguza msongamano wa mizigo bandarini”, alisema Minhajj.

Alifafanua kuwa, mfumo wa TeSWS unawawezesha wafanyabiashara kukamilisha maombi ya vibali na maandalizi ya malipo ya kodi za forodha kidijitali, bila kwenda kwenye taasisi mbalimbali za udhibiti wa forodha, hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Minhajj aliongeza kuwa, mfumo wa TeSWS umeleta mapinduzi makubwa katika utendaji kazi wa shughuli bandarini, hivyo kupunguza msongamano wa shehena bandarini na kuongeza uwazi hasa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali

Alibainisha kuwa, kupitia mfumo wa Single Window, mteja anaweza kuwasilisha taarifa zake kieletroniki na hatimaye kuondoa usumbufu kwa mteja kulazimika kufika au kuzunguka ofisi moja hadi nyingine kufuatilia hatua za shehena ya mzigo wake.

“Kupitia Mfumo huu watumiaji wa bandari wanaweza kuwasilisha taarifa zao na kufanyiwa kazi kwa haraka zaidi lakini pia, umepunguza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali” alisisitiza Minhajj.

Aidha, Minhajj alibainisha kuwa, TPA imekuwa ikishirikiana vizuri na e-GA katika utengenezaji wa miongozi ya ndani ya TEHAMA na kuhakikisha wataalamu wa ndani wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara, ili kuimarisha udhibiti na usalama wa mifumo ya taasisi hiyo.

Aidha, alitaja baadhi ya mifumo inayotumika katika utendaji kazi wa TPA ambayo ni zao la e-GA kuwa ni pamoja na Mfumo wa Barua pepe Serikalini (GMS), Mfumo wa kuomba vibali vya safari nje ya nchi (e-Vibali) na Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) ambayo imesaidia kurahisisha mawasiliano na utendaji kazi ndani na nje ya taasisi hiyo.

Katika kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA, Minhajj alisema kuwa TPA inafuata na kuzingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, katika ujenzi wa mifumo na miradi mbalimbali ya TEHAMA.

Sambamba na hayo, Minhajj aliishauri e-GA, kuongeza ujuzi kwa wataalamu wa TEHAMA katika teknolojia mpya ikiwemo Akili mnemba ‘Arificial Intelligence - AI’ katika ujenzi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Naye Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Sylvan Shayo alisema, e-GA imeandaa viwango na miongozo mbalimbali ya Serikali Mtandao ambayo inatoa maelekezo na taratibu zinazotakiwa kufuatwa na taasisi za umma katika ujenzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA, ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini,.

Bw. Shayo alitoa rai kwa taasisi zote za umma kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kuwa na mifumo ya TEHAMA inayoleta tija kwa Serikali na wananchi kama inavyotarajiwa.

“Taasisi zote za umma, zinapaswa kutumia kwa ukamilifu miongozo hii, ili kuleta mafanikio chanya katika utendaji kazi na utoaji wa huduma za Serikali kwa umma, na kwakufanya hivi tutakuwa tumetekeleza jitihada za Serikali Mtandao kwa ufanisi zaidi”, alisema Bw. Shayo.

Aidha, Bw Shayo aliipongeza TPA kwa ushirikiano mzuri na e-GA katika jitihada mbalimbali za ujenzi wa Serikali Mtandao na kuzitaka taasisi nyingine kuiga mfano huo ili kujenga Serikali ya Kidijitali.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict B. Ndomba, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, kwenye ufunguzi wa kongamano 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki, lililofanyika katika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

# MAZINGIRA WEZESHI YATAJWA KUCHOCHEA UKUAJI WA SERIKALI MTANDAO

Uwekezaji katika rasilimali watu, miundombinu, fedha, sera na sheria ya Serikali Mtandao, umetajwa kuwa kichocheo katika jitihada za ujenzi wa Serikali Mtandao na kurahisisha utendaji kazi Serikalini pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, wakati akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwenye ufunguzi wa Kongomano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililofanyika katika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha Septemba 9 mwaka huu.

Ndomba alisema kuwa, Serikali imeendelea kuwekeza katika jitihada za Serikali Mtandao kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo sheria, rasilimali watu, fedha na miundombinu na hivyo kuleta mafanikio makubwa yakiwemo usanifu wa mifumo mikubwa jumuishi na ya kimkakati inayotumika katika taasisi mbalimbali za Serikali.

“Serikali ya awamu ya sita, imeweka mazingira wezeshi kwetu sisi e-GA ambao tumepewa dhamana ya kusimamia TEHAMA Serikalini, ikiwa ni pamoja na kupata fedha za uendeshaji wa taasisi na miradi mikubwa ya TEHAMA ya kitaifa, kupata mafunzo ya mara kwa mara ya kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA pamoja na mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao”, alisema Ndomba.

Kutokana na uwekezaji huo, e-GA kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma imefanikiwa kujenga na kusanifu mifumo muhimu ya kitaifa ikiwemo Mfumo wa Kusimamia Malipo ya Serikali (GePG), Mfumo Jumuishi wa Malipo ya Papo Hapo (TIPS), Mfumo wa Uondoshaji Shehena maeneo ya Forodha (TeSWS), Mfumo wa Barua Pepe za Serikali (GMS) na Mfumo wa Ajira Serikalini (Ajira Portal), alisema Ndomba.

“Mifumo mingine ni ule wa Kusimamia Rasilimaliwatu (HCMIS), Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Maji na Utoaji wa Ankara za maji (MAJIIS), Mfumo wa Kusimamia Utoaji wa Huduma za Serikali kwa Njia ya Simu za Mkononi (mGOV), pamoja na Mfumo wa Kusimamia Ununuzi wa Umma (NeST)”, alifafanua Ndomba.

Sambamba na hilo, Ndomba alitoa rai kwa taasisi za umma kujiunga katika Mfumo Mkuu wakubadilishana Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus – GovESB), ili taasisi hizo kubadilishana taarifa kidijitali kama ambavyo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akielekeza taasisi za umma kubadilishana taarifa kidijiti.

Alibainisha kuwa, hadi Septembe 9, mwaka huu taasisi za umma 164 zimeshaunganishwa, na Mifumo 159 inabadilishana taarifa kupitia mfumo huu wa GovESB, miongoni mwa taasisi hizo ni Taasisi za Haki Jinai (Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa -TAKUKURU, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka - NPS na Mahakama).

Kongomano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lilifanyika kwa siku nne (04) Kuanzia Septemba 09 – 12 mwaka huu jijini Arusha, ambapo e-GA ilikuwa ni miongoni mwa wadhamini wa kongamano hilo.

> **“Ili kuwa na Serikali Mtandao madhubuti, ubadilishanaji taarifa kidijitali ni kiungo muhimu hivyo nitumie nafasi hii kutoa rai kwa taasisi ambazo bado hazijajiunga na mfumo wa GovESB kutekeleza maelekezo ya Mh. Rais kwa kujiunga na mfumo huu ili ziweze kubadilishana taarifa kidijitali ”**
>
> Mhandisi Benedict Ndomba.
> **Mkurugenzi Mkuu e-GA**




Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb).

# e-GA YAPONGEZWA UJENZI WA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI SERIKALINI

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kutengeneza mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa fedha za Serikali ambayo imesaidia kuzuia upotevu wa fedha za umma.

Mhe. Sangu alisema hayo Septemba 05 mwaka huu, wakati alipotembelea Makao Makuu ya Ofisi za e-GA zilizopo Mtumba jijini Dodoma, na kufanya mazungumzo na watumishi wa e-GA, ikiwa ni ziara yake ya kwanza katika ofisi hiyo tangu kuteuliwa kwake.

Alisema kuwa, e-GA imefanya kazi nzuri ya kusanifu na kutengeneza mifumo inayoisaidia Serikali katika ukusanyaji wa maduhuli na kuchangia kudhibiti mianya ya rushwa na upotevu wa fedha za umma.

“Kupitia mifumo mliyotengeneza e-GA, kwa sasa sisi kama Serikali tunaweza kukusanya fedha vizuri kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwani, kupitia mifumo ya kielektroniki fedha zote huenda Serikalini, hivyo jukumu linalobaki ni sisi viongozi na watumishi wa umma kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kwa weledi”, alisema Mhe. Sangu.

Aliongeza kuwa, katika kuhakikisha mifumo inayotengezwa inakuwa thabiti na kuleta matokeo chanya kwa serikali, ni lazima watumishi wa e-GA wanaotengeneza mifumo hiyo waendelee kuwa wazalendo na waadilifu kwa kufanya kazi kwa maslahi mapana ya Taifa na kutoa ushirikiano unaohitajika kwa Serikali.

“Vilevile, niwapongeze e-GA kwa kusanifu na kutengeneza mifumo ya TEHAMA inayotumika katika taasisi mbalimbali za umma ambapo, hapo awali mifumo hiyo ilikuwa inatengenezwa na wakandarasi jambo ambalo limesaidia kuokoa fedha nyingi za Serikali”, alisisitiza Mhe. Sangu.

Aliitaja baadhi ya mifumo iliyotengenezwa na e-GA na inatumika katika taasisi mbalimbali za umma kuwa ni pamoja na Mfumo wa Barua Pepe za Serikali (GMS), Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), na Mfumo wa Malipo Serikalini (GEPG), na kuitaka e-GA kuendelea kuisimamia vyema mifumo hiyo na kuimarisha usalama wake ili iendelee kufanya kazi vyema zaidi.

Sambamba na hilo, Mhe. Sangu aliitaka e-GA kufanya mapitio na tathmini ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma, ili kuhakikisha Taasisi za Umma zinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao.

“Najua mnafanya kazi vizuri lakini, nawakumbusha kuwa mnapaswa kuendelea kufanya tathmini ya miradi mbalimbali ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha taasisi zote za umma zinazingatia Sheria ya Serikali Mtandao, Viwango na Miongozo ili miradi hiyo ilete tija kwa Serikali”, alisisitiza Mhe. Sangu.

Alifafanua kuwa, ikiwa Taasisi za Umma zitazingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika hatua za uanzishwaji wa miradi mbalimbali ya TEHAMA , itasaidia kuondoa urudufu wa mifumo na kuokoa fedha za Serikali.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, alimshukuru Mhe. Sangu kwa ziara hiyo na kuahidi kutekeleza maelekezo yote aliyotoa ikiwa ni pamoja na kuimarisha uadilifu na uzalendo kwa watumishi wa e-GA.




Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakati alipofanya ziara katika Ofisi za e-GA ziizopo Mtumba Jijini Dodoma.




Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Subira Kaswaga, akizungumza na waandishi wa Habari wakati wa maonyesho ya Saba Saba yaliyofanyika Mwezi Julai Jijini Dar Es Salaam.

# WAHAMASISHENI WADAU WENU KUTUMIA MFUMO WA e-MREJESHO KUWASILISHA KERO ZAO

Taasisi za umma nchini, zimetakiwa kuwahimiza wadau wake kutumia mfumo wa e-Mrejesho kuwasilisha kero na maoni mbalimbali, sambamba na taasisi hizo kuhakikisha zinashughulikia maoni na kero hizo kwa wakati, kupitia mfumo wa e-Mrejesho ili kuendelea kujenga imani kwa wadau wake.

Wito huo umetolewa na Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Subira Kaswaga, wakati wa Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara maarufu kama 'Sabasaba' yaliyofanyika katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam.

Subira alisema, e-GA imetengeneza mfumo wa e-Mrejesho kwa lengo la kuiwezesha Serikali kupokea malalamiko, maoni na pongezi kutoka kwa wananchi ili taasisi za umma ziweze kujitathmini juu ya utendaji kazi wake kupitia mfumo huo pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Mfumo huu umekuwa jukwaa na kiungo muhimu cha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi wake, hivyo ni muhimu taasisi za umma zihamasishe wananchi na wadau wake wote kutumia mfumo huu kuwasilisha kero au maoni yao, lakini pia taasisi nazo zihakikishe zinashughulikia maoni hayo kwa wakati na kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo", alisema Subira.

Itakumbukwa kuwa Juni 26 mwaka huu, mfumo wa e-Mrejesho ulishinda tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 'UN Public Service Innovation Awards' na kutambuliwa kuwa jukwaa muhimu la mawasiliano kati ya Serikali na wananchi ambalo pia huisaidia Serikali kufanya maamuzi ya kisera kwa wakati.

"Taasisi za umma zinaweza kujitathmini juu ya utendaji wake kupitia mfumo huu kwa kubaini maeneo ambayo yanalalamikiwa kwa wingi na wateja wake ambao ni wananchi na maeneo ambayo yanayoridhisha na hivyo kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi ya kisera kwa wakati", alifafanua Bi. Subira.

Aliongeza kuwa, e-GA itaendelea na ubunifu wa kutengeneza mifumo mbalimbali kwa lengo la kuzisaidia taasisi za umma kuweza kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati na urahisi zaidi kupitia TEHAMA. kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza.

"Tutaendelea na tafiti pamoja na bunifu mbalimbali za TEHAMA lakini pia lazima tuhakikishe hatuko nyuma kwenye teknolojia zinazoibukia (Emerging Technologyies) hivyo, tutahakikisha kuwa teknolojia hizi zinazoibukia tunazitumia vema kuhakikisha zinaleta mchango chanya kwenye Serikali", alisema Bi. Subira.

Naye mmoja wa wananchi waliotembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Andrew Munare, alieleza kufurahishwa na huduma zinazotolewa na e-GA sambamba na kujifunza namna ya kupata huduma mbalimbali za Serikali kwa haraka kupitia mfumo wa huduma za serikali kwa simu ya mkononi (m-Gov).

"Nimefurahi kupata elimu kuhusu huduma za e-GA na kufahamu uwepo wa mfumo wa kutuma malalamiko, maoni na mapendekezo (e Mrejesho), ambao unatuwezesha sisi wananchi, kutuma malalamiko na mapendekezo Serikalini kwa haraka zaidi na kufuatilia malalamiko hayo tukiwa mahali popote kupitia simu ya mkononi" alisema Bw. Munare.

Hali kadhalika Bw. Charles Paul Nazi alibainisha kuwa, wananchi wamekuwa wakihangaika juu ya namna bora ya kuwasilisha maoni na malalamiko yao hivyo, kupitia mfumo wa e-mrejesho wananchi wataweza kuwasilisha malalamiko yao na kuwasiliana moja kwa moja na taasisi husika.

Mfumo wa e-Mrejesho umesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), unasimamiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# na kisha kuchagua namba 8 na kisha namba 2, njia zingine ni kupitia simu janja kwa kupakua Aplikesheni (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana kwenye Play Store na Apple Apps Store, na kwa njia ya Tovutiya emrejesho.go.tz.

# KUTOKA KITUO CHA UTAFITI, UBUNIFU NA UENDELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO



Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhendisi Benedict Ndomba, akizungumza na wanafunzi wanaoshiriki programu ya mafunzo kwa vitendo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025.



Wanafunzi wanaoshiriki programu ya mafunzo kwa vitendo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 katika kituo cha eGOVRIDC wakisikiliza hotuba kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA.

## JIFUNZENI TEKNOLOJIA MPYA KWA MASLAHI YA TAIFA:MHANDISI NDOMBA

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi, Benedict Ndomba, amewataka wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini katika fani ya TEHAMA, kutumia fursa hiyo kujikita zaidi katika kuzielewa teknolojia mpya zinazoibukia ili kuhakikisha zinaleta tija kwa Taifa.

Ndomba ameyasema hayo Septemba jijini Dodoma, wakati akifungua programu ya mafunzo kwa vitendo (practical training) kwa mwaka wa fedha 2024/2025, inayoendeshwa na Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GovRIDC).

"Teknolojia mpya zinaibuka kila mara duniani, hivyo mnapokuwa hapa mtumie nafasi hii kujifunza na kubuni vitu vipya kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza, lakini ni lazima muhakikishe vitu vyote mnavyobuni vinakuwa na maslahi mapana kwa Taifa" alisema Ndomba.

Alieleza kuwa, e-GA kupitia e-GovRIDC imekuwa ikiendesha mafunzo hayo kila mwaka kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wa fani ya TEHAMA kutoka vyuo mbalimbali kupata ujuzi na uzoefu pamoja na kufahamu hali ya soko la ajira ilivyo ili waweze kushindana katika soko la ajira kimataifa.

"Kwa upande wa mafunzo kazini 'Internship' na nafasi za wanaojitolea, tunao watumishi waliosoma ndani na nje ya nchi, kituo hiki kinatoa nafasi kwa Mtanzania yeyote aliyepo ndani na nje ya nchi mwenye shauku ya utafiti na ubunifu kuwasilisha maombi yake kupitia mfumo wa Ubufuni (ubunifu.ega.go.tz)", amefafanua Ndomba.

Aliongeza kuwa, madhumini ya e-GovRIDC ni kufanya tafiti kwenye eneo la Serikali Mtandao na TEHAMA kwa ujumla, sambamba na kuwajengea uwezo vijana wazawa kupitia programu mbalimbali zikiwemo za mafunzo kwa vitendo, mafunzo kazini na nafasi za kujitolea kwa kushirikiana na Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini na Nje ya nchi.

Aidha, Ndomba aliwataka vijana hao kutumia teknolojia mpya katika kubuni mifumo itakayoongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi.

"Ni matarajio yangu kuwa kila mmoja wenu atashiriki kikamilifu katika kuzielewa na kuzitumia teknolojia hizi kwakuwa huu ndio uelekeo wa dunia sambamba na hilo mtaweza kubuni mifumo mbalimbali kupitia teknolojia hizo", alisema Mhandisi Ndomba.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji wa e-GA Bw.Salum Mussa, aliwapongeza vijana hao kwa kupata fursa ya kushiriki katika programu hiyo na kuwataka kutumia fursa hiyo kupata ujuzi na uzoefu utakaowasaidia kufanya vema zaidi watakaporejea vyuoni.

Aidha, Meneja wa eGovRIDC Mhandisi. Dkt. Jaha Mvulla, alisema kuwa mafunzo hayo kwa mwaka huu yamejikita zaidi katika kuzielewa teknolojia mpya zinazoibukia 'Emerging Technology' kama vile Akili Bandia 'Artificial Intelligence', Sarafu ya Kidijitali 'Digital Currency', Block Chain, Usalama wa Mtandao 'Ciber Security' na 'Internet of Things (IOT) na kuangalia namna ambavyo teknolojia hizo zitaweza kuisaidia Serikali katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Dkt. Mvulla alifafanua kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha vijana hao wanazielewa teknolojia mpya zinazoibukia na kupata uzoefu na ujuzi wa kutosha wa matumizi sahihi ya teknolojia hizo.

Kwa upande wake Meneja wa Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Raphael Rutaihiwa amewakumbusha vijana hao kuzingatia maadili ya utumishi wa umma wakati wote wanapokuwa katika mafunzo hayo ikiwa ni pamoja na mavazi, weledi, uadilifu na nidhamu.

Bi. Glory Baraka, mwanafunzi wa mwaka wa pili (2) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alieleza matarajio yake kuwa ni kujikita katika eneo la Akili Mnemba (Artificial Intelligence - AI) na kutumia ujuzi huo katika ushindani wa soko la ajira.

Naye Bw. Frank Mhoja mwanafunzi wa mwaka wa pili (2) Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ameishukuru e-GA kwa kupata fursa ya kushiriki mafunzo hayo ambayo anaamini yatawasaidia kuzielewa teknolojia mpya na kutumia teknolojia hizo katika uvumbuzi wa mifumo mbalimbali itakayosaidia Serikali katika utendaji kazi.

Programu hiyo maalumu ya mafunzo kwa vitendo, ilihusisha wanafunzi 65 kutoka vyuo kumi na mbili 12 Tanzania bara na Visiwani, mafunzo hayo yalifanyika kwa muda wa wiki 10.

# MATUKIO KATIKA PICHA

**ARUSHA:** Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb), akimkabidhi cheti cha Shukrani ya Udhamini wa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba katika Ukumbi wa AICC Jijini Arusha.








Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict B. Ndomba, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwenye ufunguzi wa kongamano 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililofanyika katika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

# KARIBU OFISI ZA e-GA



Naibu Waziri Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), akisalimia na Mkurugenzi mkuu wa Mamalaka ya Serikali Mtandao Mhandisi Benedict Ndomba, mara baada ya kuwasili katika ofisi za e-GA Mtumba Jijini Dodoma.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), akisalimiana na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) alipofanya ziara katika Ofisi hizo.




Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), akisaini kitabu cha wageni.

# MAONYESHO ZANZIBAR

Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakitoa elimu ya Serikali Mtandao na huduma zitolewazo na Mamlaka, kwa wanachi waliotembelea banda la e-GA katika mkutano wa 3 wa Tathmini na Ufuatiliaji (The 3rd Tanzania Monitoring,Evaluation and Learning Conference) uliofanyika Zanzibar.



**MTUMBA:** Wanafunzi wanaoshiriki mafunzo kwa vitendo katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GovRIDC), wakiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya e-GA walipofanya ziara katika ofisi za e-GA Mtumba Jijini Dodoma .







**DODOMA:** Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imetoa Mafunzo ya kupitia maboresho yaliyofanyika na moduli mpya zilizotengenezwa katika mfumo wa Dawati la Msaada (HelpDesk System) yaliyofanyika September 2024 Jijini Dodoma.



Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA Bw. Ricco Boma




Washiriki wa Mafunzo ya Mfumo wa Dawati la Msaada



Meneja wa Huduma kwa Wateja Bw. Long'ida Oltetiai



Washiriki wa Mafunzo ya Mfumo wa Dawati la Msaada wakipewa mafunzo ya Mfumo huo na Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw. Faraja L. Mpande.

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI

Mhandisi Benedict B. Ndomba
Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE

Salum Mussa
Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

SACP Hamis Ali
Meneja Ukaguzi wa Ndani

SACP Raphael Rutahiwa
Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai
Meneja wa Huduma kwa Wateja

## MHARIRI

Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano

## WAANDISHI


Catherine Peter | Afisa Habari **Mwandamizi**
Queenter Mawinda | Afisa Habari **Mwandamizi**

## WAPIGA PICHA

Mussa Enock |Afisa Habari
Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA

Edger Msamba | Afisa TEHAMA




ISO 9001: 2015 CERTIFIED

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Ofisi ya Rais,**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao,**
S.L.P 2833, Dodoma.

**Tovuti :** www.ega.go.tz
**Barua pepe :** info@ega.go.tz